

Waziri Ulega mnada wa samaki uko wapi?

Niliona taarifa ya samaki kuuzwa kwa njia ya mnada katika Soko la Samaki Feri jijini Dar es Salaam.

Bila shaka hatukuwa na mnada, lakini kwa mujibu wa vyombo vya habari mnada haujafanyika na hao samaki wametoweka. Lakini inasadikiwa kuna mtu aliyepewa samaki hao na mtu huyo anafahamika.

Naomba kukuuliza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, huo mnada wa samaki uliousema uko wapi, mbona haujafanyika?

Mauna, 0658252377, Dar es Salaam



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema
ubia kati ya sekta za umma na binafsi katika kukuza shughuli
za kilimo nchini umeimarika.

JAMHURI UK 4.

Ulega agusia 'PPP' *

kuinua kilimo

DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema
ubia kati ya sekta za umma na binafsi katika kukuza shughuli
za kilimo nchini umeimarika.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa 15
wa Chama cha Wachumi Kilimo Tanzania (AGREST) wiki
iliyopita, Ulega amesema kupitia ubia huo mafanikio zaidi
katika kilimo yatapatikana

"Ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya
uongozi madhubuti wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan
kupitia Wizara ya Kilimo, kwani hatua zimechukuliwa
kuhakikisha sekta binafsi inatoa mchango stahiki kwenye
uzalishaji," amesema.

Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa kilimo
kimeliingizia taifa takriban dola za Marekani bilioni 1.4
kwa mazao yaliyouzwa nje, hivyo kuwa sekta muhimu kwa
maendeleo ya uchumi.

Amesema kilimo biashara kikizingatiwa sambamba na
ushauri wa wataalamu, kitatoa mchango mkubwa katika
kukuza pato la mkulima mmoja mmoja na la taifa.

Mkutano huo umejadili namna bora ya kutatua
changamoto zinazo~~ikabili~~ sekta ya kilimo, zikiwamo bidhaa
kuyafikia masoko, teknolojia na ubunifu, ushiriki wa vijana,
upatikanaji wa fedha, ubia kati ya sekta za umma na binafsi
(PPP) na uongezaji wa thamani kwa mazao.

Mwenyekiti wa AGREST, Dk. Florens Turuka, amesema
kilimo kinachangia asilimia 35 ya thamani ya uchumi katika
Afrika, huku kwa dunia kikiwa na mchango wa asilimia 50.

"Mnyororo wa thamani wa shughuli zinazoimarisha
kilimo ni muhimu sana. Ni zaidi ya uzalishaji katika kilimo.
Kwa mfano, kilimo kwa Tanzania kinachangia asilimia 26 ya
pato la taifa (GDP). Vilevile kinachangia asilimia 65 ya ajira,"
amesema Dk. Turuka.

Dk. Turuka ambaye ni mtaaluma mbobezi wa uchumi
kilimo, anasema kilimo ni chanzo muhimu cha chakula, ajira,
kipato na malihi za viwandani.

"Asilimia 50 ya maisha ya wakazi katika Bara la Afrika
wanategemea kilimo," amesema.

* Waliovamia kongani za malisho mifugo wapewa siku 7 waondoke *

Na Paul Mabeja, KITETO

SERIKALI imetoa siku saba za kuondoka watu wote waliovamia na kufanya shughuli za kilimo kwenye maeneo ya kongani za malisho ya mifugo zilizotegwa kuititia mpango wa matumizi bora ya ardhi za vijiji wilayani Kiteto mkoani Manyara.

Watakaokaidi agizo hilo baada ya muda huo, itaendeshwa operesheni ya kuwaondoa kwa nguvu watu wote waliovamia maeneo hayo na kuwafikisha mahakmani.

Mkurugenzi Msaidizi wa Uendelezaji Maeneo ya Malisho Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Gabriel Bura alitoa maagizo hayo juzi wakati wa kikao cha viongozi wa kimila wa jamii ya Kimasai na Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kilichofanyika wilayani hapa.

Bura alisema maeneo hayo ya kongani za malisho kwa

ajili ya mifugo yalitengwa kwa mujibu wa sheria, hivyo watu wote ambao wamevamia hivi sasa na kufanya shughuli nyininge tofauti na ufugaji wanatakiwa kuondoka mara moja.

"Ninatoa siku saba watu wote wawe wameondoka kwani maeneo yale yametengwa kwa ajili ya ufugaji tu na si kitu kingine na kwa yule ambaye atafanya shughuli nyininge zaidi ya ufugaji anavunja sheria.

"Mpango wa matumizi bora ya ardhi nchini umefanyika kwa asilimia 45 na maeneo ambayo yametekeleza zaidi ni Manyara na Arusha. Hapa kwenu mpango umefanyika ni jukumu lenu kuzilinda hizi kongani za malisho. Sheria ya Malisho inakataza maeneo haya mtu kulima, kujenga au kuchimba madini," alisitisiza.

Alisema kuwa katika kipindi hicho cha siku saba, watu wote wanapaswa kuondoka bila kujali ni wafugaji au wakulima.

"Nitoe wiki moja viongozi wote wanaofanya shughuli yoyote ambayo haihusiki kisheria watoke kwani wote ni wavamizi bila kujali walikotoka.

"Pia niwaombe ninyi wafugaji kuwa walini wa maeneo haya kwani ninyi ndio mme-kuwa mnawakaribisha watu kwenye hizi kongani za malisho," aliagiza.

Mwenyekiti wa Malaigwanani (viongozi wa kimila wa kabilo hilo) Wilaya ya Kiteto, Emmanuel Sinogoro, aliomba serikali kuchukulia hatua za kisheria dhidi ya baadhi ya wafugaji waliokaidi agizo la kutoka kwenye maeneo ya nyanda za malisho.

Alisema hali hiyo itasaidia kuondokana na kero ya maeneo ya malisho katika wilaya hiyo inayosababisha migogoro ya muda mrefu baina ya wafugaji na wakulima.

Sinogoro alisema kuwa moja ya sababu zinazochangia

maeneo ya malisho kuvamiwa ni wafugaji wenye kumaribisha watu kwa ajili ya shughuli za kilimo kwenye kongani za malisho.

"Hivyo basi, tunaomba iundwe timu iende kubaini watu wote waliovamia ili waondolewe kama ambavyo tulikubaliana sisi wafugaji tuwe wa kwanza kuachia maeneo hayo yalitengwa kwa ajili ya kongani za malisho," ali-sisitiza.

Makamu Mwenyekiti wa CCWT, Kusundwa Wamalwa, alisema kuwa baada ya kipindi hicho cha siku saba, wataziomba mamlaka husika kuchukua hatua kali kwa wataokaidi agizo hilo.

Alisema ili jamii ya wafugaji nchini ipate mafanikio inapaswa kushirikiana kwa kila jambo ikiwamo kipinga vitendo vyta unyanyanyasaji vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa serikali na askari wa mapori ya akiba nchini.



WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wa pili kulia) akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella (katikati) na viongozi wengine baada ya kufungua Tamasha la Utalii 2023, wilayani Chato, juzi.

Ulega urges financiers: Invest in Lake Victoria zone tourism

By Guardian Correspondent, Chato

MINISTER for Livestock and Fisheries Abdallah Ulega has encouraged investors to tap innumerable tourism investment opportunities in the lake zone including Chato District to massively promote tourism in the area.

Ulega made the call yesterday here when speaking at the inauguration of the 'Chato Utalii Festival 2023' which aims at promoting tourism and marketing investment opportunities available in Geita region.

He said that there lots of tourism

potentials in the lake zone and Geita Region in particular that are yet to be tapped "that's why I'm encouraging investors from all corners of the world to come and in tourism value chain."

He said that the region boasts an array of natural wonders including forests, waterfalls, mountains and savannahs which are home to various species such as elephants, lions, zebras and giraffes.

Apart from Burigi Chato National Park, Ulega also mentioned one of the most popular tourist-relevant sights in Geita as Rubondo Island National Park.

He stated that the festival carries

various investment concepts, especially in terms of agriculture, livestock and fishing, tourism, culture and sports.

Ulega further mentioned various sectors that have investment opportunities in the region noting that the government has injected 1.7bn/- for the construction of a storage facility and a large modern fish market in Chato district which will provide commercial opportunities and increase the value of fish and seafood products.

He added that the government has also injected 1.8bn/- for construction of a large facility to process fish at Rubambagwe

located in Chato district which will enable fishermen to fish in cages in Lake Victoria.

Ulega also said the ministry has built a modern livestock auction in Buzirayombo, which provides an opportunity for livestock keepers to conduct their livestock businesses.

He stated that the presence of a good number of livestock provides another opportunity to build a meat processing plant.

The minister mentioned other areas with opportunities as the construction of hotels of three-to-five-star status, saying plots are available in Chato district.

According to him, the government also intends to practice irrigation, since a large part of the Chato district is surrounded by Lake Victoria and the construction of textile factories due to the presence of cotton.